

Kuwasaidia watu wa Victoria kupata mahitaji yao ya nishati ya siku zijazo

Kudumisha usalama wa nishati ni muhimu tunapohamia katika siku zijazo zenye kaboni ya chini. Hapo ndipo gesi itaendelea kuwa na jukumu muhimu. Viva Energy kwa sasa inaendesha kiwanda cha kusafisha mafuta huko Geelong, kama sehemu ya Kituo cha Viva Energy. Tunapendekeza kituo kipywa kando ya kiwanda cha kusafisha mafuta ili kuleta kwa urahisi Gesi ya Kimiminika (LNG) Victoria. Kusini-mashariki mwa Australia inatarajiwa kukabiliwa na uhaba wa gesi asilia katika miaka ijayo. Kituo chetu kinaweza kupokea LNG kwa magari ya mizigo maalum kutoka kaskazini mwa Australia au nje ya nchi. Hii itahakikisha usambazaji salama, ulio mwepesi wa gesi wakati na mahali inapohitajika zaidi.

Taarifa kuhusu mchakato wa uidhinishaji wa udhibiti

Mnamo 2022, tulitayarisha Taarifa ya Athari za Mazingira (EES) kwa ajili ya Serikali ya Victoria. Taarifa hii ilitoa taarifa juu ya athari mbaya za mazingira zinazoweza kutokea kutokana na mradi. Jopo lililoitishwa na serikali lilitathmini EES, na kufanya mkutano wa hadhara.

Mnamo 2023, Waziri wa Mipango aliomba Viva Energy kuandaa Taarifa ya Nyongeza. Tuliulizwa habari zaidi kuhusu athari zozote zinazoweza kutokea kwa mazingira .

Taarifa ya Nyongeza sasa inapatikana kwa ukaguzi wa umma na kuwasilishwa.

Ufikiaji kamili kwa www.vivaenergy.com.au/gas-terminal-supplementary-statement

Inatoa maelezo zaidi juu ya athari zinazoweza kutokea kutokana na ujenzi na uendeshaji wa Kituo cha Gesi. Pia inaeleza jinsi athari zozote mbaya zingepukwa au kupunguzwa. Ili kukamilisha kazi hii, tulifanya tafiti za kina katika maeneo manne yaliyoainishwa hapa chini.

Mazingira ya Baharini

Kulinda mazingira ya bahari ni kipaumbele kwa Viva Energy. Wataalamu huru walitathmini ikolojia ya baharini, ubora wa maji na athari zinazoweza kutokea kwa wanyamapori.

Kazi zaidi ilifanyika ili kuelewa vyema mazingira yaliyopo. Hii ni pamoja na athari za utiririshaji wa maji taka uliopo kutoka kwa kisafishaji.

Ubora wa Hewa

Utafiti wa awali ulihitimisha kuwa athari za ubora wa hewa zitakuwa za chini, za ndani na kuzingatia kanuni. Tulifanya majaribio zaidi ya unyeti kwenye uundaji wa asili.

Kelele

Wataalamu walifuatilia kelele katika maeneo manane ya karibu wakati wa mchana, jioni na usiku. Hii ilikuwa kutathmini viwango vya kelele vilivyopo na kukokotoa vikomo vya kelele vinavyofaa. Vikomo hivi vililinganishwa na kelele inayotarajiwa kutoka kwa ujenzi na uendeshaji wa kituo.

Urithi wa Utamaduni wa Waaboriginal

Mtaalam wa kujitegemea alihusika kukamilisha tathmini ya kiakiolojia ya kitamaduni ya Waaboriginal chini ya maji. Hii ilifanyika ili kutambua maeneo ya urithi wa kitamaduni wa Waaboriginal katika eneo hilo.

Tutaendelea kufanya kazi na Wamiliki wa Jadi ili kudhibiti athari za urithi wa kitamaduni.

Kuhusu Kituo cha gesi kilichopendekezwa

Mradi huu utatoa usambazaji wa gesi kwa gharama nafuu na rahisi kusini-mashariki mwa Australia.

Kituo cha gesi kitajumuisha:

- Upanuzi wa Gati iliyopo ya Kusafisha mafuta katika Bandari ya viwanda ya Geelong;
- Meli inayojulikana kama Kitengo cha Kuelea cha Hifadhi na Urekebishaji (FSRU) ilisimama kwenye Gati, inayotolewa na wabebaji (magari makubwa) wa LNG;
- Kituo cha matibabu kilicho ndani ya tovuti ya kusafisha Geelong; na,
- Bomba la kilomita 7 kutoka FSRU hadi kituo cha unganisho la mtandao huko Lara.

Kwa taarifa zaidi

energyhub@vivaenergy.com.au

1800 515 093

 [geelongenergyhub](https://www.facebook.com/geelongenergyhub)

vivaenergy.com.au/energy-hub



Changanua msimbo ili kusajili na kupokea masasisho ya mradi

Ikiwa ungependa maelezo zaidi au kuuliza maswali ya timu yetu ya mradi, junge nasi kwenye kikao cha jumua.

Jumatano tarehe 25 Septemba 2024
Saa 4:30 Asubuhi – Saa 7:30 mchana
(10:30am - 1:30pm)

Maktaba ya Geelong
51 Little Malop St, Geelong

Tutatoa muhtasari wa jumla wa mradi. Pia tutajadili mchakato wa vibali vya udhibiti na masomo ya mazingira.

Jumatano tarehe 2 Oktoba 2024
Saa 9 alasiri – 12:30 jioni
(3pm - 6:30pm)

Maktaba ya Waurn Ponds
230 Pioneer Rd, Grovedale